




LIDA Stories

lidastories.net

Mume mzee / Un uomo anziano
per marito


✎ Aranya
☑ Sunniva Høiby-Øiset
📄 Jacob Haule (sw), Andrea Ciasca Marra
(it)



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>

Mume mzee

Un uomo anziano per marito



✎ Aranya
☑ Sunniva Høiby-Øiset
📄 Jacob Haule
|| 5


☺ Kiswahili / Italiano 



Nilifikiri wanaume wa Norwei ni wanaume bora duniani, lakini hii si kweli! Kabla sijaonana na mwanaume ambaye alikuja kuwa mume wangu, nilikuwa ninafanya kazi kiwandani Bangkok na yeye aliishi Pattaya. Tulikutana mtandaoni na hatimaye tukawa wapenzi.

. . .


Io pensavo che gli uomini norvegesi fossero i migliori del mondo, ma non è vero! Prima di incontrare l'uomo che sarebbe diventato mio marito, io lavoravo in fabbrica a Bangkok, e lui viveva a Pattaya. Ci siamo conosciuti su internet e infine ci siamo messi insieme.



Baada ya muda tukaamua kuoana. Ninatoka
katika familia maskini, kwa hiyo kuwa na mume
kutoka nchi nyingine ambaye atahudumia
familia yangu ilikuwa ni miongoni mwa sababu
za kuolewa nae.

...

Dopo un po' abbiamo deciso di sposarci. Io
provengo da una famiglia povera, e avere un
marito straniero che si prendesse cura della mia
famiglia è stata una delle ragioni per cui l'ho
sposato.



Tuliamia Norwei na nilianza kwenda shule kujifunza Kinorwei. Ulikuwa ni wakati mgumu sana. Sikuwa na leseni ya udereva na mume wangu akawa ananipeleka shuleni, ananisubiri na ananirudisha nyumbani. Ilikuwa ni umbali wa saa moja. Baada ya muda, tuliamia karibu lakini alisisitiza kuendelea kunipeleka shuleni. Hakutaka nitembee peke yangu.


...

Ci siamo trasferiti in Norvegia e io ho iniziato a andare a scuola per imparare il norvegese. È stata davvero dura. Non avevo la patente, così mio marito doveva portarmi a scuola in macchina, aspettare che io finissi e poi riportarmi a casa. La scuola era a un'ora di macchina da casa. Dopo un po' ci siamo trasferiti più vicino, ma lui comunque insisteva per portarmi in macchina alla scuola. Non voleva che ci andassi a piedi da sola.

Sielewi hata itakuwaje, mpango wangu ni kwenda shule nyingine lakini mume wangu hapendi nifanye hivyo. Ana mpango wa kuniongezea ugomu. Ninataka kupinga lakini sijui nafanyaje, si rahisi kuishi katika nchi ya ugenini na mume mzee kama nilivyofikiri.

...


Non so cosa accadrà in futuro. Io progetto di frequentare un'altra scuola ma mio marito non vuole. Pensa di trasferirsi ancora più lontano per rendermi le cose più difficili. Vorrei resistere, ma non so come. Non è facile come pensavo vivere in un paese straniero con un vecchio per marito.




Sikuwahi kuwa na pesa tangu nihamie Norwei. Mara moja, mume wangu alinipa pesa kwa ajili ya chakula cha mchana lakini kwa sababu ni pesa kidogo, niliweka kando. Rafiki zangu shuleni walitaka kunisaidia nipate kazi lakini mume wangu alisema haiwezekani. Hafikiri!! kama kufanya kazi ya usafi ni kazi inayokubalika kwangu.

...

Da quando sono venuta in Norvegia raramente ho soldi. Una volta mio marito mi ha dato del denaro per il pranzo, ma io l'ho messo da parte, dal momento che ne avevo così poco. I miei amici a scuola vogliono aiutarmi a trovare lavoro, ma mio marito dice che non posso. Pensa che lavorare come donna delle pulizie non sia appropriato per me.






Badala yake, alinitafutia kazi nyingine, kujenga gereji. Alikuwa boshi na nilifanya kila kitu. Alikuwa hawezi kufanya makubwa kwa sababu alikuwa mgonjwa. Hakuwahi kunipa pesa aliyoipata kutokana na kazi ya kujenga gereji.

...

Lui invece aveva un altro lavoro per me: costruire un garage. Lui dirigeva i lavori e io facevo tutto quello che diceva. Non poteva far molto perché non stava bene. Non mi ha mai dato un soldo di quelli che ha ricavato dal garage.



Siku moja alisema kuwa anahisi upweke akiwa peke yake nyumbani. Kwa hiyo, tuliamua kuwa na mbwa. Sikutaka mbwa kwa sababu nilikuwa nimechoka baada ya kutoka shule na nilikuwa na kazi nilizopewa nizifanye nyumbani. Alisema ataweza kumtembeza mbwa kila siku lakini mwishowe nililazimika kuwahudumia wote, mbwa na mume wangu mzee.

...

Un giorno mi ha detto che si annoiava a stare da solo a casa, così ha deciso di prendersi un cane. Io non volevo un cane perché dopo la scuola ero stanca e avevo dei compiti da fare. Lui diceva che avrebbe portato a spasso il cane ogni giorno, ma alla fine ho dovuto occuparmi io sia del mio anziano marito che del cane.